06

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI KWA ZANZIBAR, JUNI, MWAKA 2023

OFISI YAMTAKWIMU MKUU WASERIKALI ZANZIBAR

**Utangulizi**
Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.


Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (12).

**Lengo**
Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

**Ajali za Barabarani**

Jumla ya ajali 12 zimeripotiwa mwezi wa Juni, 2023. Wilaya Kati, na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Juni 2023**




Idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Juni, 2023 zina idadi sawa na ajali zilizotokea kwa mwezi wa Mei ambapo zimeripotiwa ajali 12 kwa kila mwezi.

Kwa mwezi wa Juni 2023, wilaya Kati na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya ikilinganishwa na Mwezi wa Mei ambapo Kaskazini 'B', Wete na Micheweni ziliripotiwa kutokea ajali nyingi (2) kwa kila wilaya.


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Mei 2023 na Juni 2023**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka uliopita zimeongezeka kutoka ajali tano (5) kwa mwezi wa Juni 2022 hadi ajali 12 kwa mwezi wa Juni 2023.


Kwa mwezi wa Juni, 2023, wilaya Kati na Magharibi “B” zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya ikilinganishwa na Mwezi wa Juni 2022 ambapo wilaya ya Micheweni iliripotiwa kuwa na ajali nyingi (2).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Juni 2022 na Juni 2023**





Jumla ya waathirika 25 wameripotiwa mwezi wa Juni, 2023, ambapo waathirika 24 walikuwa wanaume na muathirika mmoja (1) alikuwa wanawake. Wilaya ya Magharibi “B” imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ambao ni 13 sawa na asilimia 52.0 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Juni 2023**





Waathirika waliofariki kwa mwezi Juni wameongezeka kwa asilimia 66.7 kutoka waathirika waliofariki sita (6) kwa mwezi wa Mei 2023 hadi waathirika waliofariki 10 kwa mwezi wa Juni 2023.

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Mei 2023 na Juni 2023**




Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi uliopita wamepungua kutoka waathirika waliojeruhiwa 22 kwa mwezi wa Mei 2023, hadi waathirika 15 waliojeruhiwa mwezi wa Juni, 2023.

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Mei 2023 na Juni 2023**





Waathirika Waliofariki kwa mwaka uliopita wameongezeka, kwa mwezi wa Juni 2022 walikuwa waathirika waliofariki wanne (4) wakati kwa mwezi wa Juni, 2023 walikuwa waathirika 10 waliofariki.

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Juni 2022 na Juni 2023**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwaka uliopita wameongezeka ambapo kwa mwezi wa Juni 2022 hakukuripotiwa majeruhi wakati kwa mwezi wa Juni, 2023 walikuwa majeruhi 15.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Juni 2022 na Juni 2023**




Waathirika wengi inaonekana ni Wapanda baskeli na pikipiki. Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki), Abiria ni 11, Wapanda baskeli na pikipiki 12 na Waendao kwa miguu wawili (2).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Juni 2023**





Kwa mwezi wa Juni 2023, ajali zaidi zilitokea muda wa saa 12:01 jioni - 3:00 asubuhi ambapo zimeripotiwa ajali nne (4) na 9:01 - 12:00 jioni zimeripotiwa ajali tatu (3).

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Juni 2023**




Jumla ya ajali 12 zilizoripotiwa mwezi wa Juni, 2023 kati ya hizo, ajali saba (7) zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali tano (5) zimesababishwa na uzembe wa madereva. Mkoa wa Kusini Unguja unaongoza kuwa na ajali zilizosababishwa na mwendo kasi (ajali 5) na Mjini Magharibi unaongoza kua na ajali zilizosababishwa na uzembe wa madereva (ajali 3).

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa Juni 2023**




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 3,175 yameripotiwa mwezi wa Juni, 2023, ambapo makosa 3,172 yameripotiwa kwa wanaume na makosa matatu (3) yameripotiwa kwa wanawake. Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 743) sawa na asilimia 23.4 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.

Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 34 (asilimia 1.1) kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Juni 2023**




Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Juni, 2023 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 953) yakifuatia na Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 720), Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia (makosa 708) na Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helment (vespa/pikipiki/fifti) (makosa 306).

Orodha ya makosa haya manne (4) ya barabarani kati ya yote 10 yaliyoripotiwa yamechangia asilimia 84.6.


Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani,Juni 2023



Idadi ya makosa kwa mwezi uliopita imepungua kwa asilimia 12.3 kutoka makosa 3,620 mwezi wa Mei 2023 hadi 3,175 mwezi wa Juni 2023.


Wilaya ya iliongoza kwa mwezi wa Mei 2023(makosa 894) na pia wilaya ya Kati imeongoza kwa mwezi wa Juni 2023 (Makosa 743).

**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Mei 2023 na Juni 2023**




Idadi ya makosa kwa mwaka uliopita imeongezeka kwa mwezi wa Juni, 2023 ambapo kwa mwezi wa Juni 2022 yaliripotiwa makosa 2,227 wakati kwa mwezi wa Juni 2023 yameripotiwa makosa 3,175.Wilaya ya Magharibi “A” iliongoza zaidi kwa makosa ya barabarani (makosa 490) kwa mwezi wa Juni, 2022 ambapo wilaya Kati imeongoza kwa mwezi wa Juni 2023 (makosa 743).

**Kiel elezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Juni 2022 na Juni 2023**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (12). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 12 zimeripotiwa mwezi wa Juni, 2023. Wilaya Kati, na Magharibi “B” zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya.
Mlinganisho wa idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Juni, 2023 zina idadi sawa na ajali zilizotokea kwa mwezi wa Mei, 2023 ambapo zimeripotiwa ajali 12 kwa kila mwezi.

Jumla ya makosa 3,175 yameripotiwa mwezi wa Juni, 2023, ambapo makosa 3,172 yameripotiwa kwa wanaume na makosa matatu (3) yameripotiwa kwa wanawake. Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 743) sawa na asilimia 23.4 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Juni, 2023 ni “Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani” (makosa 953).

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Juni 2023**

| Wilaya | Idadi ya ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Kati | 4 | 33.3 | 4 | 0 | 4 | 40.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 4 | 0 | 4 | 16.0 |
| Kusini | 1 | 8.3 | 1 | 0 | 1 | 10.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 4.0 |
| Mjini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 8.3 | 1 | 0 | 1 | 10.0 | 3 | 0 | 3 | 20.0 | 4 | 0 | 4 | 16.0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 33.3 | 4 | 0 | 4 | 40.0 | 8 | 1 | 9 | 60.0 | 12 | 1 | 13 | 52.0 |
| Wete | 2 | 16.7 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 3 | 0 | 3 | 20.0 | 3 | 0 | 3 | 12.0 |
| Micheweni | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Chake chake | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Mkoani | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| **Zanzibar** | **12** | **100** | **10** | **0** | **10** | **100** | **14** | **1** | **15** | **100** | **24** | **1** | **25** | **100** |

## Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Juni 2023

| Wilaya | Idadi ya ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda baskeli na pikipiki | | | | | | Waendao kwa miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 6 | 1 | 7 | 3 | 0 | 3 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **12** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **2** | **0** | **2** | **8** | **1** | **9** | **6** | **0** | **6** | **6** | **0** | **6** | **2** | **0** | **2** | **0** | **0** | **0** |

## Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Takwimu za Ajali Barabarani kwa Mwezi wa Juni 2022 na Juni 2023

| Wilaya | Idadi ya ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 | Juni - 22 | Juni - 23 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 4 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kusini | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 1 | 0 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 4 | 0 | 9 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **5** | **12** | **0** | **15** | **4** | **10** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **9** | **0** | **2** | **0** | **6** | **2** | **6** | **0** | **0** | **2** | **2** |

## Jadweli 3.3: Mlinganisho wa Takwimu za Ajali Barabarani kwa Mwezi Mei 2023 na Juni 2023

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda baskeli na pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 1 | 4 | 2 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 4 | 0 | 9 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Wete | 1 | 2 | 2 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 1 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 0 | 10 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **12** | **12** | **22** | **15** | **6** | **10** | **2** | **0** | **2** | **0** | **10** | **9** | **1** | **2** | **7** | **6** | **1** | **6** | **3** | **0** | **2** | **2** |

**Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Juni 2023**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji hatari | | | Ubovu wa vipando | | | Kuendesha chombo cha motobila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 5 | 0 | 5 | 17 | 0 | 17 | 58 | 0 | 58 | 224 | 0 | 224 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 2 | 0 | 2 | 4 | 0 | 4 | 32 | 0 | 32 | 108 | 0 | 108 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 113 | 0 | 113 | 4 | 0 | 4 | 238 | 0 | 238 | 212 | 0 | 212 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 31 | 0 | 31 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 39 | 0 | 39 | 110 | 0 | 110 | 40 | 0 | 40 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 69 | 0 | 69 | 94 | 0 | 94 | 30 | 0 | 30 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 114 | 0 | 114 | 77 | 0 | 77 | 16 | 0 | 16 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 1 | 0 | 1 | 15 | 0 | 15 | 56 | 0 | 56 | 7 | 0 | 7 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 23 | 0 | 23 | 3 | 0 | 3 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 12 | 0 | 12 | 40 | 0 | 40 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 3 | 18 | 8 | 0 | 8 | 9 | 0 | 9 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **20** | **0** | **20** | **121** | **0** | **121** | **303** | **3** | **306** | **708** | **0** | **708** | **720** | **0** | **720** |

## Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Juni 2023

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 | 15 | 225 | 0 | 225 | 3 | 0 | 3 | 552 | 0 | 552 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 146 | 0 | 146 | 2 | 0 | 2 | 300 | 0 | 300 |
| Kati | 7 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 76 | 0 | 76 | 91 | 0 | 91 | 0 | 0 | 0 | 743 | 0 | 743 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 0 | 25 | 124 | 0 | 124 | 3 | 0 | 3 | 187 | 0 | 187 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 57 | 0 | 57 | 0 | 0 | 0 | 115 | 0 | 115 | 0 | 0 | 0 | 361 | 0 | 361 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 42 | 0 | 42 | 113 | 0 | 113 | 0 | 0 | 0 | 348 | 0 | 348 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 0 | 31 | 60 | 0 | 60 | 0 | 0 | 0 | 298 | 0 | 298 |
| Wete | 11 | 0 | 11 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 7 | 32 | 0 | 32 | 0 | 0 | 0 | 139 | 0 | 139 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 34 | 0 | 34 |
| Chake chake | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 30 | 0 | 30 | 30 | 0 | 30 | 0 | 0 | 0 | 137 | 0 | 137 |
| Mkoani | 8 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 13 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 | 73 | 3 | 76 |
| **Zanzibar** | **31** | **0** | **31** | **57** | **0** | **57** | **251** | **0** | **251** | **953** | **0** | **953** | **8** | **0** | **8** | **3,172** | **3** | **3,175** |

**Jadweli 3.5: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni, 2022 na Juni, 2023**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji hatari | | Ubovu wa vipando | | Kuendesha chombo cha motobila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni,bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi yaabiriana mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 4 | 5 | 3 | 5 | 3 | 17 | 46 | 58 | 65 | 224 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 38 | 3 | 0 | 2 | 9 | 4 | 4 | 32 | 52 | 108 |
| Kati | 0 | 0 | 17 | 2 | 67 | 113 | 49 | 4 | 37 | 238 | 85 | 212 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 4 | 25 | 0 | 9 | 31 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 67 | 39 | 225 | 110 | 20 | 40 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 76 | 69 | 308 | 94 | 32 | 30 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 83 | 114 | 217 | 77 | 18 | 16 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 10 | 3 | 1 | 14 | 15 | 26 | 56 | 10 | 7 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 10 | 23 | 13 | 3 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 12 | 0 | 40 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 18 | 21 | 8 | 13 | 9 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **59** | **20** | **73** | **121** | **325** | **306** | **919** | **708** | **317** | **720** |

**Inaendelea… Jadweli 3.5: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni, 2022 na Juni, 2023**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 | Juni 2022 | Juni 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 15 | 66 | 225 | 0 | 3 | 195 | 552 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 21 | 3 | 68 | 146 | 0 | 2 | 192 | 300 |
| Kati | 7 | 7 | 0 | 0 | 18 | 76 | 5 | 91 | 0 | 0 | 285 | 743 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 25 | 29 | 124 | 0 | 3 | 74 | 187 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 57 | 40 | 0 | 50 | 115 | 0 | 0 | 402 | 361 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 42 | 52 | 113 | 0 | 0 | 490 | 348 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 31 | 25 | 60 | 0 | 0 | 369 | 298 |
| Wete | 0 | 11 | 0 | 0 | 7 | 7 | 51 | 32 | 0 | 0 | 111 | 139 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 2 | 4 | 4 | 0 | 0 | 35 | 34 |
| Chake chake | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 30 | 0 | 30 | 0 | 0 | 0 | 137 |
| Mkoani | 0 | 8 | 0 | 0 | 8 | 20 | 21 | 13 | 0 | 0 | 74 | 76 |
| **Zanzibar** | **7** | **31** | **0** | **57** | **156** | **251** | **371** | **953** | **0** | **8** | **2,227** | **3,175** |

## Jadweli 3.6: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Mei 2023 na Juni 2023

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji hatari | | Ubovu wa vipando | | Kuendesha chombo cha motobila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni,bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiriana mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni i2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni i2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni i2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 1 | 5 | 4 | 5 | 0 | 17 | 30 | 58 | 208 | 224 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 2 | 3 | 10 | 2 | 2 | 4 | 72 | 32 | 93 | 108 |
| Kati | 0 | 0 | 31 | 2 | 391 | 113 | 13 | 4 | 217 | 238 | 117 | 212 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 4 | 15 | 0 | 51 | 31 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 39 | 60 | 110 | 22 | 40 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 69 | 0 | 94 | 113 | 30 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 39 | 114 | 24 | 77 | 17 | 16 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 1 | 16 | 15 | 92 | 56 | 25 | 7 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 15 | 23 | 0 | 3 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 20 | 23 | 12 | 19 | 40 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 18 | 13 | 8 | 18 | 9 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **34** | **20** | **405** | **121** | **191** | **306** | **561** | **708** | **683** | **720** |


**Inaendelea… Jadweli 3.6: Takwimu za Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Mei na Juni 2023**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 | Mei 2023 | Juni 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 146 | 0 | 217 | 15 | 0 | 225 | 0 | 3 | 606 | 552 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 38 | 3 | 197 | 146 | 0 | 2 | 414 | 300 |
| Kati | 7 | 7 | 0 | 0 | 23 | 76 | 95 | 91 | 0 | 0 | 894 | 743 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 105 | 25 | 94 | 124 | 0 | 3 | 275 | 187 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 57 | 38 | 0 | 103 | 115 | 0 | 0 | 249 | 361 |
| Magharibi 'A' | 34 | 0 | 0 | 0 | 56 | 42 | 186 | 113 | 0 | 0 | 420 | 348 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 84 | 0 | 0 | 31 | 206 | 60 | 0 | 0 | 370 | 298 |
| Wete | 0 | 11 | 0 | 0 | 9 | 7 | 28 | 32 | 0 | 0 | 170 | 139 |
| Micheweni | 0 | 0 | 8 | 0 | 1 | 2 | 6 | 4 | 0 | 0 | 32 | 34 |
| Chake chake | 2 | 5 | 0 | 0 | 14 | 30 | 12 | 30 | 0 | 0 | 96 | 137 |
| Mkoani | 6 | 8 | 0 | 0 | 18 | 20 | 13 | 13 | 0 | 0 | 94 | 76 |
| **Zanzibar** | **49** | **31** | **238** | **57** | **519** | **251** | **940** | **953** | **0** | **8** | **3,620** | **3,175** |


**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Juni 2023**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 552 | 13,686,000 |
| Kaskazini 'B' | 300 | 6,123,900 |
| Kati | 339 | 11,397,000 |
| Kusini | 187 | 3,072,000 |
| Mjini | 278 | 25,315,150 |
| Magharibi 'A' | 318 | 40,377,750 |
| Magharibi 'B' | 204 | 39,942,000 |
| Wete | 130 | 2,426,500 |
| Micheweni | 33 | 713,000 |
| Chake chake | 116 | 4,930,000 |
| Mkoani | 71 | 1,196,000 |
| **Zanzibar** | **2,528** | **149,179,300** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani za Barabarani Zilizoripoti kwa Wilaya, Juni 2023**



**Kielelezo 2:Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya, Juni 2023**



**Zingatia Maelezo**

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua, 2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136